

K.C.S.E 2005 KISWAHILI KARATASI YA 102/3

SEHEMU A: TAMTHILIA

S.A. Mohamed: Kitumbua Kimeingia Mchanga
Alamin Mazrui: Kilio cha Haki

S.A. Mohamed: Kitumbua Kimeingia Mchanga
Jibu swali la 1 au la 2.

1. "Mwandishi wa tamthilia ya kitumbua kimeingia mchanga amemchora mwanamke kama kikwazo katika harakati za kujikomboa". Fafanua kauli hii ukitoa mifano mitano. (alama 20)
2. "Na utaja mpaka lini? Mwezi mzima unalia....."
 - (a) Fafanua muktadha wa maneno haya (alama 2)
 - (b) Mhusika anayelia anahuzunishwa na nini? (alama 8)
 - (c) Anayelia ana maoni tofauti na mzungumzaji kuhusu swala wanalozozania. (alama 10)

Alamin Mazrui: Kilio cha Haki
Jibu swali la 3 au la 4.

3. (a) Eleza mambo yote muhimu yaliyotokea katika kiosk cha Mzee Ingeli wakati wateja walipoingia. (Alama 14)
- (b) Kwa nini Lanina na Mzee Ingeli walihuzunika kuhusu yaliyomfika mtu wa 4? (alama 6)
4. "Ah mwanangu wee! Dunia hii huisha maneno?
Kila mmoja asema lake,
na babaako...ameanza kuathirika sasa."
 - (a) Baba anaathiriwa na mambo gani? (alama 8)
 - (b) Punde tu baada ya mazungumzo haya kunatokea nini? (alama 12)

SEHEMU B: RIWAYA

Mohamed S. Mohamed: Kiu
Katama Mkangi: Walenisi
Jibu swali la 5 au la 6

5. Huku ukizingatia matukio yote katika safari ya utu, tofautisha tabia ya Dzombo kwa upande mmoja na tabia za Mtu - Bint Fikirini na Mtu - Wazo kwa upande mwingine. (alama 20)
6. "Dzombo machozi yasiyozuilika yakamdondoka. Ni nani aliyesema mbinguni hakuna machozi? Mtakatifu huyo..."
 - (a) Huzuni aliyokuwa nayo Dzombo ilitokana na nini? (alama 12)
 - (b) Mtu Bint Hekima na Mtu - Bint Fikirini walikuwa na maoni gani kuhusu swala la mapenzi baina ya wanaume na wanawake Jehanamu? (alama 8)

Mohamed S. Mohamed: Kiu

Jibu swali la 7 au la 8.

7. Kwa kurejelea ndoa ya Bahati, fafanaa desturi zinazozingatiwa wakati wa arusi. (alama 20)
8. "Nikienda shitaki kwetu baba ananitoa mbio ananiambia: tokamea huko huko, usije na maneno ya kipumbavu hapa, nyie wanawake wanajulikana mlivyo."
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 10)
- (b) Kutokana na muktadha wa wa maneno haya.
- (i) Wanawake wanajulikana vipi? (alama 5)
- (ii) Kwa nini wanawake hawapaswi kushtakia matatizo yao? (alama 5)

SEHEMU C: Ushairi

9. Soma mashairi yafuatayo kisha ujibu maswali.

Shairi A

Shairi B

- | | |
|---|--|
| 1. Mpenda cha bure boza, tenaje ni baradhuli
Tamaaye humpumbaza, huzidi kuwa jahili,
Vya bure humwongoza, kwa wengine ajidhili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari | 1. Hana wema binadamu, usimuone kucheka
Acheke akusalimu, moyoni hutukutika
Japo maneno matamu, upate kupambazika,
Akheri sumu ya nyoka, binadamu kazidia. |
| 2. Bure kweli hulemaza, tena ina sumu kali,
Epuka vinaumiza, sana vyaleta ajali
Kooni takukwaruza, ijapo vina samli,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari. | 2. Binadamu madhulumu, usidhanie dhihaka,
Nyoka kweli ana sumu, umwonapo waepuka,
Binadamu ni vigumu, hawezi kuepukika,
Akheri sumu ya nyoka, binadamu kazidia. |
| 3. Sikitu cha kwendekeza, falau kuwa asali,
Cha bure kimepooza, ijapo embe kwa wali
Kiache kina mafunza, hata kitiwe achali,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari. | 3. Binadamu hudhulumu, kumbe huku akicheka,
Moyonimwe ana sumu, kali kushinda ya nyoka,
Asikione kitamu, mkononi umeshika,
Akheri sumu ya nyoka, binadamu kazidia. |
| 4. Wenye hekima hupuza, huona kitu dhalili,
Na hufanywa kimeoza, kinamfaa tumbili,
Waungwana hukibeza, kwao hakisitahili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari. | 4. Mbele yako tabasamu, wala hutaona shaka,
Kumbe kwako ni hasimu, atamani kukuzika
Akupake marihamu, kilio akianguka,
Akheri sumu ya nyoka, binadamu kazidia. |
| 5. Cha mahonyo hutatiza, pato hilo siyo mali,
Ndio mlango wa kiza, geuka siukabili,
Utalingia Gereza, jumba lisilo kandili,
Bure ina sumu kali, yafaa kujihadhari. | 5. Binadamu madhulumu, na maneno yangu shika,
Utafika kwa Hakimu, ukifikiri dhihaka,
Na mengine mashutumu, gerezani kutumika,
Akheri sumu ya nyoka, binadamu kazidia. |

- (a) Linganisha dhana ya 'sumu' kama inavyojitokeza katika mashairi haya mawili (A na B). (alama 4)

- (b) Eleza maana ya mishororo ifuatayo kama ilivyotumiwa katika mashairi haya.
- (i) Kooni takukwaruza, ijapo vina samli. (alama 1)
- (ii) Cha bure kimepooza, ijapo embe kwa wali. (alama 1)

- (iii) Acheke akusalimu, moyoni hutukutika. (alama 1)
 (iv) Kumbe kwako ni hasimu, atamani kukuzika. (alama 1)
 (c) Fafanua dhana ya 'gereza' katika shairi A na B. (alama 4)
 (d) Andika ubeti wa 4 katika shairi A kwa lugha nathari. (alama 4)
 (e) Dondoa na uandike maneno mawili kutoka shairi 'A' na mengine mawili kutoka shairi 'B' ambayo yameendelezwa kimakusudi ili kutosheleza mizani. (alama 4)

10. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

1. Moyoni furaha sina, ningaitaka sinayo
 Si usiku si mtana, ni mambo kwangu hayo
 Mateso nnayoona, yajijua wangu moyo
 Si mwako na wayowayo, uliyonifikiliya!
2. Nna jipu linfunza, linipalo tabu mno
 Tangu nionianza, kamwe sipati usono
 Kwamba ni mara ya kwanza, kuuguwa ndwezi hino
 Latoma kama sindano, utunguwe nakwambiya
3. Si jana wala si juzi, liliponianza tangu
 Ni mingi mno miezi, nnadhofu hali yangu
 Nnakonda kama uzi, kwa kushitadi utungu
 Kubwa tumaini langu, ni mwishowe nangojeya
4. Hitaka keti siwezi, kwamba li makaliyoni
 Kutwa huwa yangu kazi, kusimama; ntendeni?
 Na usiku usingizi, siupati aswilani
 Kucha nakesha mwendani, kwa utungu kuzidiya.
5. Kili kipele mwilini, ndiyo mwanzo wake kuwa
 Sikujuwa aswilani, kuwa jipu chaja kuwa
 Nngekijuwa zamani, ningekitangiya dawa
 Ni kwamba sikutambuwa, ndipo hakiwatiliya.
6. Siku ya kuiva kwake, hiyo ndiyo siku kweli
 Huo ndiwo mwisho wake, na mwisho wa idhilali
 Idhilahi in'ondoke, mimi nayo tuwe mbali
 Siku hiyo ni mawili, kuteka au kuliya
7. Taliminya litumbuke, lisisumbuwe tena
 Usaha wote utoke, utoke nikiuona
 Midamu itiririke, kama ng'ombe alonona
 Jipu hili mwana lana, Mn'gu mbwalipa hizaya
8. Baada ya yote haya, jahara niliuguze
 Kwa madawa kulitiya, ili kwamba yalipoze
 Irudi yangu afiya, na zaidi niongeze
 Nirukeruke niteze, kwa furaha kuningiya.

- (a) Fafanua mambo yanayomkera msanii wa shairi hili. (alama 4)
 (b) Onyesha matumaini ya msanii katika shairi. (alama 4)
 (c) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathari. (alama 4)
 (d) Dondoa mfano mmoja wa tashbihi na mwingine wa balagha. (alama 2)
 (e) Katika ubeti wa 5 mshairi anajuta. Eleza. (alama 3)
 (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi.
 (i) wayowayo.
 (ii) kushitadi.
 (iii) idhilali (alama 3)